محمد ﷺ خاتم النبيين - سواحيلي

# Muhammad ﷺ ndio Nabii wa mwisho




جمعية الدعوة بالزلفي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

286

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ ـ فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# Muhammad (SAW) ndio Nabii wa Mwisho

محمد þ خاتم النبيين – سواحيلي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
هاتف: 164234466 966 ـ فاكس: 164234477 966

# محمد خاتم ﷺ النبيين - سواحيلي

**أعده وترجمه للغة السواحيلية**

**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**

**الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ**


ⓒ جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ

*فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر*

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
محمد خاتم النبيين / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ

٧٥ ص ؛ ..سم

ردمك: ٩٧٨-٦٠٣-٨٣٩٩-٢٠-٠

١- السيرة النبوية أ.العنوان

ديوي ٢٣٩ ١٤٤٤/٥٨٣٣

**رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨٣٣**

**ردمك: ٩٧٨-٦٠٣-٨٣٩٩-٢٠-٠**

# Muhammad Rehema na Amani Zimfikie Ndio Nabii wa Mwisho

## محمد Ý خاتم النبيين

### Hali za Waarabu Kabla ya Mtume Kutumwa:

Ilikuwa kuabudu masanamu ndio dini kubwa kwa waarabu. Kwa sababu ya kujiegemeza kwenye dini, inayokwenda kinyume na dini iliyonyooka, iliyofahamika zama zake kuwa ni dini ya kijahiliya.

Walikuwa na masanamu wao mashuhuri wakiwa abudu kinyume cha Allah ambao ni Laata, Huzza, Manata na Hubba. Pia ilipatikana baina ya waarabu ambao walifuata dini ya kiyahudi au kinaswara au kimajusi. Pia walipatikana kikundi kidogo kilichoendelea kushikamana na dini ya Nabii Ibrahim *Alayhi Ssalam*.

Kuhusu hali ya Kiuchumi, Waarabu walikuwa wakitegemea sana kutoka vijijini utajiri unaotokana na ufugaji wa wanyama. Na ulikuwa msingi mkuu wa maisha ya kiuchumi kwa watu wa mjini ni kilimo na

biashara. Ulipokaribia kuja kwa Uislamu, Mji wa Makkah ulikuwa ni kitovu cha biashara katika bara la Arabu. Kwani ulikuwa na ustaarabu wa kuimarishwa kwa majengo katika sehemu mbali mbali kama vile Madina na mji wa Twaif.

Kuhusu upande wa mambo ya kijamii. Dhulma ilikuwa imeenea kwa hali ya juu. Mtu dhaifu hana haki, watoto wa kike wakizikwa wakiwa hai na mambo ya haramu yakifanywa, mwenye nguvu akiidhulumu haki ya mtu dhaifu na wakioa wanawake wengi bila ya idadi maalumu. Uzinzi ulikithiri katika jamii. Vita kati ya makabila au ndani ya kabila moja vilitokea kwa sababu ndogo sana.

Hayo ni maelezo mafupi kuhusu bara Arabu kabla kudhihiri Uislamu.

Ibn Adhabihain amesema: "Waarabu walikuwa wakijifakharisha kwa Abdul Mutwalib, babu yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie, kwa sababu ya watoto na utajiri. Abdul Mutwalib akaweka nadhiri ya kuwa Allah Akimruzuku watoto wa kiume kumi atamchinja mmoja wao kama kafara la kujikurubisha kwa miungu wao. Yakatimia yale ambayo aliyakusudia na kuyataka. Aliruzukiwa watoto wa kiume kumi, na akawa mmoja wao ni baba yake

Mtume Rehema na Amani Zimfikie, Abdillah. Wakati Abdul Mutwalib anataka kutekeleza nadhiri yake akapiga kura kwa watoto wake nani achinjwe. Kura ikamuangukia baba yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie, Abdillah. Wakati anataka kumchinja watu wakasimama upande wake kumzuia ili isiwe kwa watu kuwa ndio taratibu yao kila mwaka kufanya hivyo.

Kisha wakaafikiana ipigwe kura kati ya Abdillah na ngamia kumi ili iwe ndio fidia yake ya kumkomboa. Walipopiga ikatokea kuwa achinjwe Abdillah. Wakawa wanazidisha idadi ya ngamia lakini ikawa kila mara kura inamuangukia Abdillah. Mpaka ikafikia idadi ya ngamia mia moja, ndipo ikaangukia kura kwenye ngamia, akawachinja. Abdul Mutwalib akatoa fidia kwa mwanae Abdillah hao ngamia.

Abdillah alikuwa ni mtoto kipenzi kwa baba yake Abdul Mutwalib, moyoni mwake, hasa hasa baada ya kumkomboa. Wakati anakua kijana baba yake alimchagulia binti wa kuoa kutoka katika kabila la Zuhrat. Bint aitwaye **Amina bint Wahbi.** Akamuozesha binti huyo. Alipata ujauzito Amina. Baada ya miezi mitatu ya mimba yake Amina, Abdillah akapata safari ya kutoka kwenda Shamu na

kundi la wafanya biashara. Na akiwa njiani anarudi akitoka safari akapatwa na maradhi ikambidi afikie kwa wajomba zake Banu Najar katika mji wa Madina. Na hapo ndipo alipofia na akazikwa katika mji wa Madina. Ilipotimia miezi ya kujifungua akajifungua mtoto wa kiume, ambaye ni Mtume Muhammad Rehema na Amani Zimfikie, siku ya Jumatatu.

Na pia wako Wanavyuoni wa Tarekhe wanaosema kuwa hakuna tarehe maalumu ya siku aliyozaliwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Inasemekana kuwa alizaliwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie, tarehe tisa ya mwezi wa Mfungo sita. Wengine wanasema alizaliwa mwezi kumi na mbili ya mfungo sita, wengine mwezi wa Ramadhani, wengine tofauti na tarehe hizo. Na mwaka wake wa kuzaliwa ulikuwa ni 571 A.D. Na huo mwaka ulikuwa ni mwaka ulioitwa mwaka wa Tembo (Tukio ambalo lilikuwa maarufu la kutaka kuvunjwa Al-Ka'aba).

## Kisa cha Tembo.

Ni kwamba Abraha Al-Habashiyyi, aliyekuwa mwakilishi wa mfalme Najashi katika mji wa Yemen, wakati alipowaona waarabu wanakwenda kuhiji mji wa Makkah na kuiadhimisha na kuitukuza Ka'aba, na wanakuja kwa wingi kutoka katika sehemu za mbali,

basi akalijenga Kanisa kubwa katika mji wa Nasa'a. Mji mkuu wa Yemen ili waweze kuacha kwenda Makkah na kuelekea Yemen kwa ajili ya Ibada. Akayasikia maneno haya bwana mmoja kutoka kabila la Banu Kinana na akaingia kanisani usiku, akajisaidia haja kubwa na akaipakaza kwenye kuta zote za lile Kanisa. Aliposikia Abraha kuwa kuna mtu amefanya kitendo hicho akakasirika sana. Na akaandaa jeshi kubwa sana lenye watu elfu sitini. Wakiwa pamoja nao ndovu tisa waliokwenda nao Makkah ili waivunje Ka'aba. Akamchagua Tembo mkubwa akampanda. Alipofikia karibu na mji wa Makkah akaliandaa jeshi ili auingie mji wa Makkah, lakini tembo alipiga magoti akakaa hakuenda. Wakawa kila wakimuelekeza njia ya kwenda Makkah anaelekea njia nyingine akikimbia. Wanapokuwa wanamuelekeza Ka'aba anapiga magoti. Wakiwa katika hali hiyo Allah Akawatuma kwao wao ndege, makundi kwa makundi, wakiwa wamebeba mawe madogo madogo, yenye moto kutoka katika moto wa Jahanam. Kila ndege amebeba mawe matatu, moja kwenye mdomo wake na mawili amebeba kwenye miguu yake. Halimpati mtu jiwe hilo isipokuwa linamkatakata viungo vyake na kumchanachana

mpaka kufa. Ilipowakuta hali hiyo wakaanza kukimbia na hali yakuwa wanaanguka njiani.

Kuhusu Abraha, Allah Alimtia maradhi ya kukatikatika vidole vyake. Hakufika katika mji wa Sana'a akawa yamempata mauti akafariki dunia. Ama Makuraishi wao walitawanyika katika mabonde na milimani wakiogopa isije ikawapata gharika kama iliyowapata watu wa Abraha. Wakarudi majumbani mwao wakiwa na Amani salama salimini. Na tukio hili lilitokea kabla ya kuzaliwa kwa Bwana Mtume Muhammad Rehema na Amani Zimfikie kwa muda wa siku hamsini.

## Kunyonyeshwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Wakati alipozaliwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie alinyonyeshwa na Thuwaibat, mtumishi wa A'ami yake Mtume, Abu Lahab. Na huyu alikuwa amekwisha mnyonyesha A'ami yake Hamza bin Abdul Mutwalib. Kwa hali hiyo Hamza akawa ni ndugu yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie katika kunyonya.

Kwani katika tabia za waarabu enzi hizo walikuwa wakiwatafuta wanawake ambao watawanyonyesha

watoto wao kutoka vijijini. Kutokana na sababu kuwa watu wa vijijini wanakua na miili iliyo salama.

Basi Mtume akahamishwa kupelekwa kwa mnyonye-shaji mwingine. Katika kipindi hicho ambacho alizaliwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie lilifika kundi la akina mama kutoka vijijini. Kutoka katika kabila la Bani Sa'ad. Wakitafuta watoto wa kuwanyonyesha. Wakiwa wanazunguka kwenye majumba mbali mbali na wote walikuwa wakimkataa Mtume Muhammad kumnyonyesha kutokana na uyatima wake na ufakiri alionao. Akawa Halimat Sa'adiyyah ni miongoni mwa wanawake hao ambao walimkataa kumnyonyesha Mtume. Lakini baada ya kuzunguka kwenye majumba mengi hakumpata mtoto yeyote wa wenye pesa kumnyonyesha. Mtoto atakayemueze -sha kupata malipo ambayo yatapunguza ukali wa maisha yake. Na hasa hasa ukiangalia mwaka huo ulikuwa ni mwaka wa njaa kali na ukame. Akafikiria sana, kisha akaamua kurudi nyumbani kwa Amina, mama yake Mtume, kuja kumchukua na kunyonyesha mtoto yatima kwa malipo madogo.

Mama Halima akawa amefika katika mji wa Makkah pamoja na mume wake wakiwa wamempanda punda

mnyonge dhaifu akitembea polepole. Wakiwa njiani wanarudi na mama Halima akiwa amemuweka Mtume kwenye chumba chake. Akawa punda anamlinda Mtume kwa kila adui anayetaka kumfanyia uadui, kila aina ya mnyama anayekuja kwa nyuma, mpaka wale ambao wanaambatana nao njiani wanashangazwa na hali hiyo. Kama alivyosimulia mama Halima kuwa matiti yake hayakuwa na maziwa isipokuwa kidogo sana, na watoto walikuwa wakilia kutokana na uhaba wa maziwa na njaa. Lakini wakati huo, alipoanza kuyanyonya, Mtume Rehema na Amani Zimfikie, yakaanza kububujika maziwa kwa wingi. Wakaanza kusema kutokana na ukame wa Ardhi yao katika nyumba ya Bani Sa'ad kuwa tumepata heshima na hadhi tokea tulipoanza kumnyonyesha mtoto huyu. Ardhi ya eneo hilo ikatoa mazao na mifugo yao ikazaa kwa wingi na hali yao ya maisha ikabadilika. Kutoka kwenye unyonge na ufukara mpaka kwenye utulivu na unafuu wa maisha.

Mtume alimaliza miaka miwili katika kunyonyeshwa na Halima na alikuwa akimpatiliza kila aina ya upatilizaji, lakini alikuwa akiona vitu sio vya kawaida kwa huyu kijana.

Na baada ya miaka miwili mama Halima alimchukua Mtume na kumpeleka kwa mama yake na babu yake katika mji wa Makkah. Lakini mama Halima aliziona Baraka za Mtume Rehema na Amani Zimfikie wakati akiwa naye. Akamsisitiza kuwa mama Amina amuache Mtume abaki aishi naye kwa mara ya pili. Mama Amina akamkubalia amchukue. Halima akarudi naye mpaka nyumbani kwao katika nyumba ya Bani Sa'ad akiwa anaye kijana yatima. Wakafurahi sana.

## Tukio la Kupasuliwa Kifua.

Siku hiyo alikuwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa amekaribia miaka minne, wakati akiwa anacheza na ndugu yake katika kunyonya, mtoto wa Halimat Sa'adiyah. Alikuja kijana wa Halima akikimbia huku akiwa na huzuni iliyotanda usoni mwake, akamtaka mama yake akamuone ndugu yake wa kikuraishi. Mama yake akamuuliza kuhusiana na hili jambo, akamwambia kwa hakika nimewaona watu wawili wamevalia nguo nyeupe wamemchukua mbele yetu na wakamlaza kisha wakampasua kifua chake. Kabla ya kukamilisha maelezo, akaenda Halima kwa Muhammad akamuona amesimama sehemu aliyokuwa, hatikisiki na huku akiwa amebadilika, uso wake umekuwa njano sana. Akamuuliza yaliyomsibu,

Mtume akamjibu anajisikia vizuri. Akamueleza kuwa alijiwa na watu wawili waliovaa nguo nyeupe wakamlaza chini na kumpasua kifua chake kisha wakautoa moyo wake. Wakatoa ndani yake kinyama cheusi wakakitupa. Kisha wakauosha moyo wake kwa maji ya baridi. Kisha wakaurudisha sehemu yake. Kisha wakapangusa juu ya kifua wakaondoka kisiri siri.

Akarudi Halima na Muhammad nyumbani kwake mpaka ilipochomoza alfajir ya siku ya pili akamchukua Muhammad akampeleka kwa mama yake katika mji wa Makkah. Walipofika mama Amina alistaajabu sana kwa kurejea Halima muda usiokuwa wenyewe, pamoja na kuwa alikuwa na pupa ya kumuona mwanae. Akamuuliza sababu ya kuja mapema ni nini, mama Halima akamuhadithia tukio la kupasuliwa mtoto kifua.

Akatoka mama Amina pamoja na mtoto mpaka mji wa Madina ili akafanye ziara kwa wajomba zake katika Bani Najar, akakaa huko siku kadhaa. Wakati wanarudi kutoka Madina kuja Makkah, mama Amina akakutwa na mauti sehemu inayoitwa Ab'waha na

sehemu hiyo ndipo alipozikwa. Hapo ndipo Mtume alipoagana na mama yake akiwa na umri wa miaka

sita. Akachukuliwa na babu yake Abdul Mutwalib akamlea na kumsimamia katika mambo yake yote.

Alipofikia miaka minane babu yake akafariki. Akachukuliwa na kulelewa na A'ami yake Abu Twalib pamoja na kuwa ana watoto wengi na uchumi dhaifu. Alikaa na A'ami yake na akawa kama mmoja wa watoto wake.

Kwa hakika kijana huyu yatima alishikamana na A'ami yake kwa muda mrefu sana. Na katika mazingira haya ndio ikadhihirika kwake mambo muhimu. Alikulia katika ukweli na uaminifu. Ikawa ndio laqabu yake wanayomuitia watu - kuwa amekuja mtu muaminifu, amefika mtu mkweli. Ndivyo alivyokuwa Mtume akifahamika hivyo.

Alipokuwa kijana mwenye umri wa ujana akawa ni mwenye kujitegemea katika mambo ya maisha yake mwenyewe. Akitafuta chumo la maisha yake. Akaanza kutafuta kazi ya kuweza kuendesha maisha yake. Akafanya kazi ya kuchunga wanyama kwa baadhi ya matajiri wa Kiquraishi na akipata malipo ya kiasi kwa ajili ya kuendesha maisha yake.

Alishiriki safari ya kibiashara kwenda Shamu. Alipewa kazi na mama Khadija aliyekuwa tajiri mwenye mali

nyingi. Aliyekuwa muwakilishi wake katika hiyo safari ni mtumishi wake mama Khadija anayeitwa Maisarah. Kwa Baraka ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie na uaminifu wake walipata faida kubwa katika biashara ya mama Khadija. Faida ambayo hawajawahi kuipata. Waliporudi mama Khadija akamuuliza kijana wake Maisarah sababu ya kupata faida kiasi hicho. Maisarah akamuambia mama Khadija kuwa Muhammad alisimamia kuuza na kuonyesha bidhaa, wakawa watu wanakuja kwa wingi kununua, ndio wakapata faida kubwa bila ya kufanya dhulma. Mama Khadija akamsikiliza kwa makini kijana wake kwani alikuwa akijua baadhi ya mambo kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie, akazidi kustaajabu. Hapo ndipo alipoingiwa na shauku ya kutaka kuolewa na Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Siku moja mama Khadija akamuuliza mmoja wa ndugu zake wa karibu kuhusu kuolewa yeye na Muhammad. Hapo Mtume alikuwa amefikia umri wa miaka ishirini na tano. Akajiwa na mwanamke kumueleza kuwa Khadija anakutaka umuoe. Mtume akakubali.

Ndoa ikakamilika. Ikapita miaka mingi mama Khadija akapata mimba akajifungua watoto, miongoni mwa watoto wake wa kike ni Zainabu, Ruqaiyya, Ummu Kuluthumi, Fatma; na Watoto wake wa Kiume ni Qassimu, Abdullah. Na watoto hawa wa kiume walikufa hali yakuwa bado ni wadogo.

## Utume.

Ilipokaribia miaka arobaini katika umri wake Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa mara nyingi akipenda kujitenga katika Jabal Hiraa. Mlima uliopo katika mji wa Makkah kwa upande wa Mashariki, huko anamaliza masiku katika kumuabudu Allah. Katika usiku wa mwezi ishirini na moja wa mwezi wa Ramadhan wakati akiwa kwenye pango na umri wake umefikia miaka arobaini akajiwa na Malaika Jibril *Alayhi Ssalam* akamwambia “Soma”. Mtume akamjibu “Sijui kusoma”. Malaika Jibril *Alayhi Ssalam* akalirudia neno hilo soma mara tatu, mara ya tatu akamwambia:

قال الله تعالى:( اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ❋ خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ❋
اقْرَأْ وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ ❋ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ❋ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ❋)

(العلق: 1–5)

*"Soma kwa jina la Mola wako Alieumba kila kitu, Amemuumba mwanadamu kutoka katika pande la damu, soma hakika ya Mola wako ni Mkarimu, Ambaye Amefundisha kwa kutumia kalamu, Amemfundisha mwanadamu yale asiyoyajua."* (Al-A'laq: 1-5).

Kisha Jibril *Alayhi Ssalam* akaondoka. Hakuweza Mtume kubakia pale pangoni akarudi nyumbani kwake akafika kwa mama Khadija huku akitetemeka, akamwambia mkewe "Nifunike! Nifunike!" Mama Khadija akamfunika mpaka uoga ulipomuondokea akamwambia mama Khadija yale yaliyomsibu kule pangoni, kisha akamwambia: "Kwa hakika nimeogopa sana." Mama Khadija akamuambia: "Sio hivyo, kwa hakika Allah Hawezi kukuacha tu hivi hivi, hakika yako weye ni mwenye kuunga udugu, na mwenye kubeba majukumu, na kuwasaidia wasiokuwa nacho, na kulisha wageni na kuwafanyia ukarimu, na mwenye kuwasaidia watu katika matatizo ya kidunia."

Baada ya muda kidogo alirudi Mtume kwenye Jabal Hiraa ili aendelee kufanya ibada zake. Alipomaliza kufanya ibada yake akatoka kurudi Makkah, alipofika kwenye uwanja mkubwa akajiwa na Jibril *Alayhi Ssalam* hali ya kuwa amekaa juu ya kiti kati ya

mbingu na ardhi, akamfunulia Mtume Rehema na Amani Zimfikie ikashuka hii sura:

قال الله تعالى: (يَا أَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ * قُمْ فَأَنْذِرْ * وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ * وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ * وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ * ) (المدثر: 1 – 5)

*"Ewe uliyejifunika nguo, simama uonye, na Mola wako umtukuze, na nguo zako uzitwaharishe, na Ibada ya masanamu uiache."* (Al-Mudathir: 1-5)

Kisha wahyi ukaendelea kushuka kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Mtu wa mwanzo kuupokea Uislamu na kushuhudia Upweke wa Allah ni mke wake Mtume, mama Khadija na ndiye akawa wa mwanzo kusilimu. Na Mtume akamueleza rafiki yake kipenzi Abubakar Allah Amuie Radhi naye akasilimu, alikubali bila ya kuwa na shaka yoyote moyoni mwake. Mtume akaenda kwa A'ami yake Abu Twalib kumlingania kwani alikuwa ndiye aliyemlea Mtume baada ya kufiwa na mama yake na babu yake, lakini hakuweza kuitikia wito wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Akasilimu Ally bin Abu Twalib aliyekuwa akimlea. Kisha akasilimu na kuifuata haki Zayd bin Haritha mtumishi wa mama Khadija.

Akaendelea Mtume kuwalingania watu kwa siri. Wakawa Waislamu wanauficha Uislamu wao. Kwani mtu akidhihirisha jambo lake la Uislamu basi Maquraish watamuadhibu kila aina ya adhabu ili atoke kwenye Uislamu na kuuwacha.

## Kulingania kwa Wazi.

Baada ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie kumaliza miaka mitatu katika kufanya da'awa ya kumpwekesha Allah kwa siri. Allah Akateremsha:

(فَاصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿) (الحجر: 94)

*"Toboa ukweli kwa yale uliyoamrishwa na uwape nyongo washirikina."* (Al-Hijri: 94)

Siku moja Mtume akasimama juu ya Jabal Swafa akawa anawaita watu wa Makkah. Wakakusanyika watu wengi kuja kumsikiliza Mtume, na miongoni mwao alikuwa Ami yake Abu Lahab ambae alikuwa ni adui yake mkubwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Walipokusanyika watu Mtume akasema kuwaambia:

((أرأيتم إن أنبأتكم أن وراء هذا الجبل عَدُوًّا يتربص بكم، أَمُصَدِقِيَّ أنتم؟)) قالوا: ما عهدنا فيك إلا الصدق والأمانة، فقال: ((إنّي لكم نذير بين يدي عذاب شديد)).

*"Hivi mnaonaje ikiwa nitawaambia kuwa nyuma ya huu mlima kuna adui anawafuatilia je, mtanisadikisha?' Wakasema: 'Hatujawahi kupata chochote kutoka kwako isipokuwa ni ukweli na uaminifu.' Akawaambia: 'Hakika yangu kwenu ni muonyaji - mbele yangu kuna adhabu kali."*

Kisha Mtume akaendelea kulingania kwa ajili ya Allah na kuwataka kuiacha ibada ya kuabudu masanamu, akajidhihirisha Abu Lahabi katika watu akasema: "Mwana kuangamia wewe, hili ndilo ulilotukusanyia hapa?" Ikashuka sura inayomuhusu Abu Lahabi ambayo itasomwa mpaka siku ya Kiyama.

(تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ * مَا أَغْنَى عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ * سَيَصْلَى نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ * وَامْرَأَتُهُ حَمَّالَةَ الْحَطَبِ * فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِنْ مَسَدٍ*)

(المسد: 1-5)

*"Imeangamia mikono miwili ya Abu Lahab naye pia ameangamia. Haitamfaa mali yake na alichokichuma.*

*Atauingia moto wenye muwako mkubwa sana siku ya kiyama. Na mke wake mbeba kuni za fitna pia atauingia moto huo; na katika shingo yake atakuwa na kamba imara atakayoburuziwa kutupwa motoni."* (Al-Masad: 1-5)

Mtume akaendelea kuwalingania watu. Akaanza kudhihirisha ulinganiaji wake katika sehemu ambazo watu wanakusanyika. Akawa anaswali kwenye Ka'aba na akawa anahudhuria sehemu wanazo kusanyika watu. Basi wanakuja washirikina kwenye masoko yao wakiwakataza watu wasimsikilize Mtume jinsi anavyo walingania watu Uislamu.

Wakadhihirisha mabaya kwa wale wote walioufuata Uislamu. Yalizidi mabaya ya Makafiri kwa yeyote mwenye kusilimu pamoja na Mtume. Yaliwapata mabaya familia ya Yassir na mkewe Sumaiyya pamoja na mtoto wao A'amar pale walipokufa wazazi wake mashahidi kutokana na adhabu kali waliyo adhibiwa na makafiri. Na akawa Sumaiyya ni

shahidi wa kwanza kufa kwa ajili ya Uislamu.

Waliadhibiwa Waislamu kwa kuamini kwao Uislamu kama vile akina Bilal bin Rabbaha aliyekuwa chini ya Umaiya bin Khalaf. Umaiya alimfanyia kila aina ya adhabu ili auache Uislamu lakini Bilal alibakia katika

*Imaan* yake na kushikamana na Dini yake. Umaiya akawa akimtoa Bilal na kwenda naye nje ya mji wa Makkah. Akiwa amemfunga minyororo na akimuwekea jiwe kubwa juu ya kifua chake, baada ya kumlaza kwenye mchanga uliopata moto, huku akimpiga fimbo yeye na wafuasi wake. Akiwa Bilal anasema: "Mungu ni Mmoja, Mungu ni Mmoja" mpaka siku moja akapita Abubakar nao wakiwa katika hali ya kumuadhibu Bilal. Abubakar Allah Amuie Radhi akamnunua na akamuacha huru kwa ajili ya Allah.

## Kuhama Kwenda Habasha.

Ilivyoendelea sababu ya washirikina katika kuwaadhibu kwa kila ambaye atadhihirisha Uislamu wake. Hasa hasa wale madhaifu miongoni mwao. Maswahaba wakamtaka Mtume waondoke kwenda Habasha kwa Mfalme Najashi kwa ajili ya kuilinda Dini yao. Kwani huko kwa Najashi watapata amani na utulivu. Kwa kuwa Waislamu wengi wanachelea nafsi zao na familia zao kutokana na maudhi ya Maquraishi kwao. Na huo ulikuwa ni mwaka wa tano katika kutumilizwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Wakahama Waislamu takribani watu sabini pamoja na wake zao. Na akawa miongoni mwao ni Uthman

bin Affan na mke wake Ruqaiyya bint wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Wakafanya kila mbinu Maquraishi kwenda Habasha kwa Mfalme Najashi kwenda kuwaharibia waislamu. Wakatuma zawadi kwa Mfalme wakimtaka awasalimishe Waislamu waliokimbilia kwake. Wakamwambia kuwa hao Waislamu wanamtukana Nabii Issa *Alayhi Ssalam* pamoja na mama yake Maryam. Najashi akawauliza Waislamu kuhusiana na hilo. Wakamuwekea wazi vile inavyosema Qur'an kuhusu Nabii Issa mwana wa Maryam, wakambainishia haki na wakamsomea *Surat Maryam*. Najashi akawapa Amani na akakataa kuwasalimisha kwa Maquraishi. Baada ya muda akasilimu Najashi na akatangaza Uislamu wake.

Katika mwaka huo huo alitoka Mtume Rehema na Amani Zimfikie kwenda kuwalingania watu sehemu ya Ka'aba. Akasimama akawa anasoma *Surat Najm*. Kukawa kuna kundi kubwa la Maquraishi lisilowahi kusikia Maneno ya Allah tangu mwanzo. Ikawa ni sababu ya kuambizana kuwa wasimsikilize Mtume na Qur'an kutokana na mpangilio wake. Kwani iliwagonga kwenye masikio yao Maneno ya Allah, akabakia kila mmoja anaisikia Qur'an hana kingine

anachosikiliza, mpaka aliposoma: *"Sujuduni na mumuabudu Allah"* akasujudu Mtume, hawakuweza kujizuia nafsi zao wote wakapomoka kusujudu.

Waliendelea Maquraishi kuipiga vita Da'awa ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie, wakatumia njia mbali mbali katika kuidhoofisha. Njia ya kuwaadhibu walioamini, kuwatenza nguvu, kuwatisha na kuwadanganya. Lakini njia zote hizo hawakufanikiwa isipokuwa Waislamu walizidi kushikamana na Dini yao ya Uislamu na kuzidi kwa watu kuingia katika Dini ya Allah.

Kisha walipoona kuwa hawajafaulu wakatafuta njia nyingine mpya ya kuupiga vita Uislamu. Wakaandika nyaraka maalumu na wakaweka sahihi wote kuwa wamekubaliana na wakaibandika ndani ya Ka'aba. Wakakubaliana kuwa wakate mawasiliano na waislamu na Bani Hashimu. Wasiuziwe wala wasinunue chochote. Wasiozeshwe wala wasipewe ushirikiano wowote. Wasiamiliwe chochote. Ikawa ni dharura kwa waislamu, wakatoka mji wa Makkah na kwenda katika sehemu za nje ya Makkah ikiitwa Shi'ib Abu Twalib. Huku walipata matatizo makubwa ya njaa. Wakatoa waliokuwa na uwezo mali nyingi katika kuwasaidia Waislamu mpaka ikafikia mama

Khadija kutoa mali yake yote. Maradhi yakatokea na ikawapelekea vitu vyao vingi kuharibika na kuangamia. Lakini waislamu walisimama kidete na kufanya subra, hakurudi nyuma hata mtu mmoja. Walikaa katika hali hiyo muda wa miaka mitatu mpaka kikasimama kikundi cha Maquraishi waliokuwa wana mafungamano ya karibu na Bani Hashimu. Wakasimama kuuvunja mkataba ule ulioandikwa kwenye zile nyaraka na wakawatangazia watu kuhusu hilo.

Wakati wakiwa wanautoa ule mkataba wao wakakuta mchwa wameula, haikubakia katika ule mkataba isipokuwa ibara moja tu iliyoandikwa: (بسمك اللهم) kikawa kifungo kimefunguliwa. Wakarudi Waislamu na Bani Hashimu katika mji wa Makkah. Maquraishi wakaendelea na msimamo wao wa kidhuluma wa kuwapiga vita waislamu.

## Mwaka wa Huzuni.

Yalianza maradhi na kutambaa katika mwili wa Abu Twalib kila sehemu na yakamlaza kitandani. Na haikuwa isipokuwa ni wakati mfupi sana akajiwa na *Sakaratil Mauti* akafariki. Mtume akiwa kichwani kwake akimtarajia kutamka *Kalimat Tauheed* لا إله إلا الله kabla ya kufariki. Lakini watu waovu waliokuwa

wamekaa pembizoni mwake wakiongozwa na Abu Jahal walimkataza asitamke hilo neno, huku wakimwambia:

أتترك دين آبائك وأجدادك، أترغب عن ملة عبد المطلب ؟

"Hivi unawezaje kuiacha dini ya baba zako na babu zako na kuiacha mila ya Abdul Mutwalib?"

Wakaendelea kumwambia hivyo mpaka akafariki kafiri katika hali ya ushirikina, ikawa huzuni ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie ni kubwa kutokana na kifo cha A'mi yake kufa kafiri.

Baada ya miezi miwili hivi kutokana na kifo cha Abu Twalibu, akafariki mke wake mama Khadija. Mtume Rehema na Amani Zimfikie akahuzunika huzuni kubwa sana. Yakazidi matatizo kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie kutoka kwa watu wake Maquraishi baada ya kufa Abu Twalibu na kufa kwa mke wake mama

Khadija Allah Amuie Radhi.

## Mtume Yupo Twaif.

Waliendelea Maquraishi na uovu wao wa kuwasalitisha na kuwaudhi Waislamu. Mtume Rehema na Amani Zimfikie akafikiria kuondoka kwenda Twaif na huku akitarajia huenda Allah

Akawaongoza kuingia kwenye Uislamu. Safari ya kwenda Twaif si jambo rahisi kwa sababu ya milima mingi iliyozunguka katika njia za kupita ili ufike. Yakawa mapokezi kwa Mtume si mazuri. Kwani hawakumsikiliza bali walimfukuza na kuwaamrisha vijana wao wamtupie mawe Mtume; mpaka wakamjeruhi kichwani na damu ikatiririka mpaka miguuni mwake. Akarudi kidogo kidogo kurudi Makkah hali yakuwa ana huzuni. Punde kidogo akajiwa na Jibril *Alayhi Ssalam* akamwambia:

(إن الله بعث إليك ملَك الجبال لتأمره بما شِئتَ)

“Hakika ya Allah Amekutumia Malaika wa Milima ili umuamrishe utakalo”.

Malaika wa milima akasema: “Ewe Muhammad ukitaka niyakutanishe majabali mawili ili niwasagesage, sema”.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie akasema: "*Bali natarajia Allah kutoa katika migongo yao wenye kumuabudu Allah Pekee bila ya kumshirikisha na chochote”.*

Na hii ndio subira kubwa aliyoifanya Mtume Rehema na Amani Zimfikie na huruma yake kwa watu wake pamoja na kuyapata maudhi makubwa kutoka kwao.

## Kupasuka kwa Mwezi.

Miongoni mwa jumla ya mijadala ya washirikina kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie walikuwa wakitaka Mtume afanye miujiza ili waweze kuthibitisha usahihi wa Utume wake. Waliyarudia rudia hayo mara nyingi. Kwa hakika walimuuliza Mtume Rehema na Amani Zimfikie siku moja kuhusu kupasuka kwa mwezi vipande viwili. Mtume akamuomba Mola wake, wakauona mwezi unapasuka vipande viwili. Maquraishi wakaiona hii dalili kwa muda mrefu lakini hawakuamini bali walisema hakika Muhammad ameturoga. Bwana mmoja akasema: "Ikiwa Muhammad amewaroga bali hawezi kuwaroga watu wote, wasubirini wapiga hesabu." Wakati walipokuja baadhi ya wapiga hesabu wakawauliza wakawajibu "Ndio, kwani tuliuona" lakini Maquraishi waling'ang'ania katika kumpinga.

## Israa na Mi'iraji.

Baada ya Mtume kutoka Twaif na aliyoyapata huko Twaif na baada ya kifo cha Abu Twalib na mama Khadija, pamoja na matatizo waliyoyapata Waislamu kutoka kwa Maquraishi, ikamjia huzuni kwenye moyo wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Katika hali hii,

ikamjia liwazo kutoka kwa Mola wake. Katika moja ya masiku alikuwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie amelala akajiwa na Jibril *Alayhi Ssalam* pamoja na *Buraq* ambaye ni mnyama anayefanana na farasi, ana mbawa mbili, anakimbia haraka sana kama umeme. Mtume akampanda kisha akaondoka naye mpaka *Baitul Maqdis* (Palestina). Kisha kutoka hapo akapanda naye mpaka mbinguni, huko akaziona alama za Mola wake nyingi na huko mbinguni ndiko alikofaradhishiwa Swala tano.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alirudi mji wa Makkah usiku huo huo akiwa na furaha na yakini moyoni mwake. Katika tukio hili Allah Anasema:

(سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَى الَّذِي بَارَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ) (الإسراء:١)

*"Ametakasika Yule Ambaye Alimtuma mja Wake usiku kutoka Msikiti wa Makkah kwenda Msikiti wa Aqswa ambao Tumeubariki pembizoni mwake, ili Tumuoneshe Alama Zetu, hakika ya Allah ni Mwingi wa Kusikia na Mwenye Kuona."* (Al-Isra: 1).

Ilipofika asubuhi akaenda Al-Ka'aba akawa anawazungumzia watu yale aliyoyaona na kuyapata

usiku ule. Makafiri wakamkanusha zaidi na kumpinga na kumfanyia masihara. Kisha wakamu-uliza baadhi ya waliohudhuria kuhusiana na Msikiti wa Aqswa. Walifanya kwa lengo la kumkwamisha. Lakini Mtume akawa anawaeleza kipengele kwa kipengele.

Washirikina hawakukomeka katika kumuuliza Mtume, wakamwambia tunataka utupe dalili nyingine isiyokuwa hiyo. Mtume Rehema na Amani Zimfikie akawaambia: *"Hakika nilikutana na msafara njiani sehemu ya Makkah."* Akawaelezea jinsi ulivyo huo msafara. Akawatajia idadi ya ngamia wake na siku watakayoingia mjini. Mtume alisema ukweli lakini Makafiri walizidi kupotea na kumfanyia inadi na kuaacha kumsadiki.

Na katika asubuhi ya siku ya kutoka Makkah kwenda Palestina alijiwa na Jibril *Alayhi Ssalam* kumfundisha namna ya kuswali Swala tano na nyakati zake. Kwani Swala kipindi hicho ilikuwa ni rakaa mbili tu asubuhi na rakaa mbili jioni.

Katika kipindi hicho Mtume alipunguza kuwalingania wale wanaokuja katika mji wa Makkah baada ya Maquraishi kupiga kelele ya kuikimbia haki. Akawa Mtume anakutana na watu katika vipando vyao na

sehemu wanazofikia akiwadhihirishia Uislamu na kuwaelezea juu ya Uislamu.

Na alikuwa A'ami yake Abu Lahab akimfuatilia na kuwatahadharisha watu na Mtume pamoja na Da'awa yake. Katika mara nyingine aliwafuata watu wa Madina akawalingania wakamsikiliza kisha akawakusanya wafuasi wake wakamuamini. Kwani kipindi hicho walikuwa watu wa Madina wakiwasikia Mayahudi wakisema kuwa kuna Nabii atatumilizwa kwa watu zama zake zikikaribia. Wakati anawalinga-nia wakajua kuwa huyu ndiye yule Mtume ambaye alikuwa akitajwa na Mayahudi, wakafanya haraka kuingia kwenye Dini ya Uislamu. Wakawa wakisema wasije kuwatangulieni kuufuata Uislamu. Walikuwa ni watu sita walio amini. Mwaka uliofuata walikuja watu kumi na mbili wanaume wakaenda kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie akawafundisha Uislamu.

Waliporudi mji wa Madina akamtuma pamoja nao Musw'abu bin U'mair ili awafundishe Qur'an na awabainishie hukumu za Dini. Kwa hakika Musw'abu aliweza kwa *Taufiq* ya Allah kuathiri jamii ya watu wa Madina. Kipindi anarudi Makkah baada ya mwaka mmoja kukaa Madina akaja na watu sabini na mbili na wanawake wawili. Mtume akakusanyika nao

wakachukua kiapo kuwa watamnusuru na kuinusuru Dini yake na kusimamia amri zake kisha wakarudi katika mji wa Madina.

## Kituo Kipya cha Da'awa.

Ukabadilika Mji wa Madina kuwa ni kituo cha Amani na haki kwa watu wake. Wakaanza Waislamu kuhamia mji huo. Maquraishi waliazimia kuwazuia waislamu kuhamia Madina. Iliwapata baadhi ya waliohama aina ya matatizo na maudhi ya Maquraishi. Wakawa wanahama kimya kimya kwa kuwaogopa Maquraishi. Ama Abubakar Swidiq Allah Amuie Radhi alikuwa akimtaka idhini Mtume ya kuhama kwenda Madina. Mtume Rehema na Amani Zimfikie akamwambia:

((لا تعجل، لعل الله يجعل لك صاحبًا))

*"Ewe Abubakar usifanye haraka, uenda Allah*

*Atakufanyia rafiki katika safari yako."*

Maquraishi uliwapata uwenda wazimu wakati walipoona Waislamu wanahama na wanakusanyika katika mji wa Madina. Ikawapa uoga kuwa jambo hili la Mtume Rehema na Amani Zimfikie linakuja juu na

da'awa yake inakuwa juu sana, wakashauriana kuhusu jambo hili.

Wakakubaliana katika kumuua Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Abu Jahal akasema: "Mimi naona tumpatie kila kijana mwenye nguvu kutoka kila kabila upanga, wakamzunguke Muhammad, kisha wampige pigo moja tu, itagawanyika fidia ya damu yake katika makabila yote yaliyoungana, wala hawataweza kusimama kufanya vita Banu Hashimu baada ya hili kupigana na watu wote."

Allah Akamuonyesha Mtume wake juu ya hii njama, akaafikiana na Abubakar kufanya hijra baada ya Allah kumruhusu Mtume ahame. Ulipofika wakati wa usiku Mtume akamtaka Ally bin Abi Twalib kulala kwenye kitanda chake ili wasielewe watu kuwa ameondoka, wajue bado yupo kitandani mwake.

Wakaja waliopanga njama wakaizunguka nyumba ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie wakamkuta Ally bin Abi Twalib amelala kwenye kitanda cha Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Wakamdhania kuwa ni Mtume wakaanza kumsubiria ili atoke wammalize na kumuua. Akatoka Mtume mbele yao na hali ya kuwa wameizunguka nyumba yake. Akawamwagia

mchanga juu ya vichwa vyao. Wakawa hawajamuona Mtume na wala hawakujua kuwa Mtume anatoka.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie akatoka kwenda kwa Abubakar Allah Amuie Radhi. Wakatoka wote wawili wakielekea upande wa Madina wakajificha katika pango la *Thauri* (*Ghari Thauri*).

Kuhusu vijana wa kiquraishi wakawa bado wanamsubiri Mtume atoke ili wamuue, wakawa katika hali hiyo mpaka ikafika asubuhi. Ilipofika asubuhi akaamka Ally kutoka kwenye godoro la Mtume, wakamuuliza yuko wapi Mtume. Ally hakuwaambia chochote kuhusu Mtume wakampiga sana lakini bila ya mafanikio. Maquraishi wakatuma maombi kila upande kwa yule atakaemleta Muhammad atapewa zawadi ya ngamia mia moja, amlete akiwa hai au amekufa.

Wakafika wanaomtafuta mpaka kwenye mlango wa pango walipojificha Mtume na Abubakar, na laiti mmoja wao angeangalia chini ya nyayo zake angewaona, ikazidi huzuni ya Abubakar kuwa safari yao haitafanikiwa. Mtume akamwambia Abubakar:

(ما ظنك يا أبا بكر باثنين الله ثالثهما. لا تحزن إنّ الله معنا)

*"Unaonaje Ewe Abubakar kwa watu wawili Allah akawa ni watatu wao? Usihuzunike hakika ya Allah Yuko pamoja nasi".*

Lakini wale watu hawakuwaona kabisa. Alikaa kwenye lile pango Mtume na rafiki yake kwa muda wa siku tatu kisha wakaondoka kuelekea mji wa Madina. Na ilikuwa njia ni ndefu na jua lilikuwa ni kali. Jioni ya siku ya pili walifika katika nyumba ya mama mmoja akiitwa Ummu Ma'abad wakamuomba chakula na maji. Hawakupata chochote, alikuwa hana kitu cha kuwapa isipokuwa kulikuwa na mbuzi aliyekonda sana akawa hata kwenda kuchunga hawezi na hana hata tone la maziwa atakapo kamuliwa. Mtume akamfuata yule mbuzi akazishika chuchu zake, mbuzi yule akaanza kutoa maziwa, akamkamua, akatoa maziwa mengi yakajaa chombo kikubwa. Ummu Ma'abad akashangaa sana kwa yale aliyoyaona. Wakanywa wote na wakatosheka kisha akamkamua mara ya pili akajaza chombo akamuachia Ummu Ma'abad wakaendelea na safari yao.

Wakawa watu wa Madina wanafuatilia kufika kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Huku wakimsubiria nje ya mji wa Madina kila siku. Ilipofika

siku ya kuwasili kwa Mtume walimpokea kwa furaha na makaribisho makubwa. Akafikia katika mji wa Qubaa katika viunga vya mji wa Madina. Akakaa hapo kwa muda wa siku nne akaanzisha hapo msikiti unaoitwa Masjid Qubaa. Na huo ukawa msikiti wa mwanzo kujengwa katika Uislamu.

Katika siku ya tano akaelekea mji wa Madina. Wakawa kila mmoja katika watu wa Madina anataka Mtume afikie kwake. Wakawa wanaishika kamba ya ngamia wake ili aelekee kwake. Mtume akawa anawaambia muacheni kwani huyo ameamriwa sehemu ya kufikia. Wakati alipofika ngamia sehemu aliyoamriwa akapiga magoti na Mtume hakushuka.

Akasimama ngamia akaenda kidogo kisha akaangalia huku na huku akarudi akapiga magoti katika sehemu yake ya mwanzo. Mtume akashuka na ikawa ni sehemu ambayo iliyojengwa msikiti wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Mtume akashukia katika nyumba ya Abu Ayub Al-Answar Allah Amuie Radhi.

Ama Ally bin Abi Twalib alikaa katika mji wa Makkah siku tatu baada ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Akaanza kuzirudisha amana za watu alizoachiwa na Mtume Rehema na Amani Zimfikie

kuzirudisha kwa wenyewe. Kisha akatoka kuelekea Madina akakutana na Mtume katika mji wa Qubaa.

## Mtume Rehema na Amani Zimfikie Yupo Mji wa Madina.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alijenga msikiti wake katika sehemu ambayo alipiga magoti ngamia. Baada ya kuinunua hiyo ardhi kwa wenye nayo. Akaanza kazi ya kuwaunganisha udugu Muhajirina na Answar. Akawafanya kila mmoja awe na ndugu yake katika Answar. Anashirikiana naye katika mali zake. Wakaanza kuamiliana pamoja na ukazidi mshikamano wa udugu kati yao.

Kwani hapo mwanzo walikuwa Maquraishi wanayo mafungamano makubwa na mayahudi wa Madina. Mayahudi walikuwa wakijaribu kuanzisha migongano na kuwafarikisha Waislamu wenyewe kwa wenyewe. Na walikuwa Maquraishi wakiwatisha Waislamu wakiwaahidi kuwamaliza kabisa. Hivi ndio ilivyokuwa hatari kwa Waislamu ya ndani na nje. Ikafikia hali hii ya kuwa Maswahaba hawalali majumbani mwao isipokuwa wamebeba silaha za vita. Kutokana na hali hii ngumu Allah Akashusha amri ya kupigana. Akaanza Mtume kutuma vikosi vya maaskari kwenda kutafuta habari na harakati za maadui. Vile vile

kwenda kuzuia misafara ya biashara ya maadui na kudhihirisha nguvu za Waislamu mpaka wajisalimishe na wawaache Waislamu na uhuru wa kuitangaza Dini yao na kuifanyia kazi. Pia Mtume alisimama katika kufunga mikataba mbali mbali na kula viapo na baadhi ya makabila.

## Vita Vya Badri.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alitia azma mara moja ya kwenda kuuzuia msafara wa kundi la wafanya biashara wa kiquraishi linalotoka mji wa Shamu. Alitoka Mtume na watu mia tatu na kumi na

tatu na alikuwa na farasi wawili na ngamia sabini tu.

Msafara wa maquraishi ulikuwa umesheheni ngamia elfu moja waliokuwa wakiongozwa na Abu Sufiyani. Alijua kuwa waislamu wametoka mji wa Madina kuja kuzuia msafara wao. Akatuma ujumbe mji wa Makkah kuwapasha habari na kutaka msaada na alibadilisha njia akapita njia nyingine. Waislamu hawakufaulu kuuzuia msafara huu.

Baada ya hapo Maquraishi walitoka na jeshi kubwa sana linalokusanya zaidi ya watu elfu moja kuja kuuokoa msafara wao. Abu Sufiyan akamtuma mjumbe kuwa msafara upo salama akawaomba

warudi Makkah. Abu Jahal akakataa kurudi wakaendelea kwenda.

Alipojua Mtume kuwa Maquraishi wametoka akataka ushauri kwa maswahaba wake, wakakubaliana wote kwenda kuwakabili makafiri wapigane nao. Siku ya ishirini na saba asubuhi ya mwezi wa Ramadhan mwaka wa pili Hijriyah pande mbili zilikutana na vita vikaanza. Vilikuwa ni vita vikali sana.

Vita hivyo viliisha kwa Waislamu kupata ushindi na kuuliwa maswahaba kumi na nne mashahidi. Na upande wa makafiri wakauwawa watu sabini na

wakachukuliwa mateka wengine sabini.

Katikati ya vita hivyo alifariki bint yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie Ruqaiya, mke wa Uthman bin Affan Allah Amuie Radhi, kwani alibakia katika mji wa Madina, yeye hakutoka kwenda vitani kwa sababu ya kumuuguza mke wake. Baada ya vita kuisha Mtume Rehema na Amani Zimfikie alimuozesha Uthman bint yake wa pili Ummu Kuluthumi. Na kwa hali hii ndipo akapewa jina Uthman la *Dhinurain* yaani mwenye nuru mbili kwa kule kuoa mabint wawili wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Baada ya vita vya Badri walirudi Waislamu mji wa Madina wakiwa na furaha kwa kupata nuru ya Allah. Wakiwa pamoja nao mateka walio wateka pamoja na ngawira walizozipata kwenye vita. Kuhusu mateka, wako waliojikomboa wenyewe kwa kutoa fidia, wako wengine walioachiwa bila ya fidia na wako wengine ilikuwa fidia yao ni kuwafundisha vijana kumi wa Kiislamu kusoma na kuandika.

## Vita vya Uhud.

Vita hivi vilitokea kati ya Waislamu na makafiri wa Makkah baada ya mwaka mmoja baada ya kutokea

vita vya Badri pale ambapo washirikina wa Makkah walipotia azma ya kuja kulipiza kisasi kwa Waislamu kwa kushindwa kwao katika vita vya Badri. Wakatoka wapiganaji elfu tatu kuja kukabiliana na Waislamu ambao idadi yao ni watu mia saba takribani. Waislamu walishinda mwanzo na washirikina wakashindwa. Wakakimbia washirikina wakielekea mji wa Makkah lakini walirudi mara ya pili ili kuja kuwamaliza Waislamu kwa kupitia mlimani ambako warusha mishale walishuka baada ya kuambiwa na Mtume wasishuke hata ikiwa waislamu watashinda au kushindwa. Wao wakashuka kutoka kwenye

mlima kuja kukusanya ngawira. Wakaupanda mlima washirikina na kuanza kuwashambulia Waislamu.

## Vita vya Handaki.

Baada ya vita vya Uhud liliondoka kundi la Mayahudi kwenda Makkah kuwahamasisha washirikina wa Makkah kuja kupigana na Waislamu katika mji wa Madina. Wakawaahidi kuwa watawasaidia, washirikina wa Makkah wakakubali hilo ombi. Kisha Mayahudi wakatoka kwenda kwa makabila mengine ya kiarabu kuwaambia hivyo hivyo nao wakakubali. Wakaanza washirikina kujiandaa na kuelekea upande wa mji wa Madina kutoka kila sehemu mpaka wakakusanyika ikafika idadi yao watu elfu kumi.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa amejua kuhusu harakati zao maadui, akawataka ushauri maswahaba zake katika hili jambo. Swahaba Salman Al-Farisiy akatoa ushauri kwa Mtume kuwa wachimbe handaki litakalouzunguka mji wote wa Madina katika sehemu ambazo hakuna milima. Wakashiriki Waislamu kuchimba handaki likatimia kwa haraka sana. Wakabaki washirikina wakipiga kambi nje ya mji wa Madina takribani mwezi mmoja, hawawezi kulivuka lile handaki.

Kisha Allah Akautuma upepo mkali kwa makafiri ukaja kung'oa mahema yao yote. Wakaingiwa na khofu wakaondoka kwa haraka wakarudi kwenye miji yao bila ya mafanikio yoyote. Allah Akavishinda vikundi Peke Yake na Akawanusuru Waislamu.

## Kuukomboa Mji wa Makkah.

Mwaka wa nane Hijriyah alipanga Mtume Rehema na Amani Zimfikie kuja kupigana vita na kuukomboa mji wa Makkah. Alitoka tarehe kumi ya mwezi wa Ramadhan akiwa na wapiganaji elfu kumi. Aliuingia mji wa Makkah bila ya upinzani wa kivita pale ambapo Maquraishi wote walijisalimisha na Allah Akawanusuru waislamu.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alielekea Msikiti Mtakatifu wa Makkah akatufu Al-Ka'aba. Kisha akaswali rakaa mbili ndani ya Ka'aba. Kisha akayavunja masanamu yote yaliyokuwa ndani ya Ka'aba na juu yake. Kisha akasimama kwenye mlango wa Ka'aba na Maquraishi wakiwa chini ya mlango wa Ka'aba wakisubiri Mtume atawafanya nini. Mtume Rehema na Amani Zimfikie

akawaambia;

يا معشر قريش، ماذا ترون أنّي فاعل بكم؟ قالوا: خيرًا، أخ كريم، وابن أخ كريم، قال: (( اذهبوا فأنتم الطلقاء)) .

*"Enyi Maquraishi! Mnaona nitawafanya nini?' Wakamjibu Mtume: "Utatufanyia mazuri, ndugu mkarimu, mtoto wa ndugu mkarimu." Mtume akawaambia: "Nendeni mmekuwa huru."*

Hapo ndipo alipopigiwa Mtume mfano mkubwa katika kuwasamehe maadui zake ambao waliwaadhibu maswahaba zake na kuwafanyia kila aina ya maudhi na kumtoa katika mji wake aliozaliwa.

Baada ya kukombolewa mji wa Makkah, waliingia watu katika Dini ya Allah makundi kwa makundi. Katika mwaka wa kumi Hijriyah Mtume alikwenda kuhiji na ikawa ndio Hija yake ya pekee aliyohiji. Mtume Rehema na Amani Zimfikie alihiji pamoja na maswahaba zaidi ya laki moja. Baada ya Hija alirudi Mtume Rehema na Amani Zimfikie katika mji wa Madina.

## Makundi Kuja kwa Mtume na Kuwaandikia Barua Wafalme.

Mambo yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie yalidhihirika na Dini ikaenea. Yakaanza kuja katika

mji wa Madina makabila kutoka kila sehemu wakitangaza kuingia kwao katika Dini ya Kiislamu.

Kama ambavyo Mtume alituma barua mbali mbali kwa watawala na wafalme akiwalingania kuingia katika Uislamu, wako miongoni mwao walioitikia wito wake na kuamini na wako wengine ambao walirudisha majibu mazuri na kutuma zawadi lakini hawakusilimu. Na wako wengine ambao walikasirika na kuchana barua ya Mtume aliyopewa kama alivyofanya Kisra mfalme wa Fursi (Iran ya sasa) ambae aliichana barua ya Mtume na Mtume Rehema na Amani Zimfikie akamlaani akasema: *"Ewe Allah Uchane chane Ufalme wake."* Haukupita muda mrefu akavamiwa na mwanaye akamuua akachukua Ufalme wake.

Kuhusu Muqaiqis Mfalme wa Misri, yeye hakusilimu lakini alimkirimu Mjumbe wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie, alimpatia zawadi amletee Mtume Rehema na Amani Zimfikie na hivyo hivyo ndivyo alivyofanya Mfalme wa Rumi Qaiswara alirudisha majibu mazuri baada ya kupewa barua na alimkirimu mjumbe wa Mtume na kumpatia zawadi.

Kuhusu Mundhir bin Saawi Mfalme wa Bahrain yeye baada ya kufikiwa na barua ya Mtume Rehema na

Amani Zimfikie aliwasomea watu wa Bahrain, wako walioamini na wako waliokataa kusilimu na kuamini.

## Kifo cha Mtume Rehema na Amani Zimfikie

Baada ya miezi miwili na nusu kutoka safari yake ya Hija, Mtume Rehema na Amani Zimfikie alianzwa na maradhi. Yakawa yanazidi siku hadi siku mpaka yakampelekea kushindwa kuwaswalisha waislamu, akamtaka Abubakar Allah Amuie Radhi awaswalishe watu.

Ilipofika siku ya jumatatu tarehe kumi na mbili ya mfungo sita katika mwaka wa kumi na moja Hijriyah, alifariki Mtume wa Allah akiwa ametimiza umri wake miaka sitini na tatu.

Zilifika habari kwa maswahaba juu ya kifo cha Mtume Rehema na Amani Zimfikie, wakakaribia kupoteza fahamu na kuchanganyikiwa. Kwani wengi wao hawakuamini kabisa juu ya kifo cha Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Mpaka akaja akasimama Abubakar akawahutubia kwa kuwatuliza na kuwabainishia ya kuwa Mtume wao alikuwa ni mwanadamu anakufa kama wanavyokufa wanadamu wengine, ndipo watu wakatulia.

Akaoshwa Mtume, akakafiniwa katika chumba cha mke wake mama Aisha Allah Amuie Radhi. Akawa Mtume ameishi miaka arobaini kabla ya Utume katika mji wa Makkah na miaka kumi na tatu baada ya Utume na akaishi miaka kumi katika mji wa Madina baada ya Utume.

Baada ya kufa Mtume Rehema na Amani Zimfikie wakakusanyika Waislamu katika kumchagua atakayechukua uongozi wa Waislamu baada ya Mtume. Wakamchagua Abubakar kuwa Khalifa wa Waislamu baada ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Akawa ni Khalifa wa kwanza katika Makhalifa wanne.

## Sifa ya Mtume Kimaumbile.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa ni mtu wa kati na kati, hakuwa mrefu sana wala mfupi. Alikuwa mpana mwenye kupangika vizuri viungo vyake na kifua kipana. Alikuwa na uso mzuri, mwenye weupe uliochanganyika na wekundu, uso wake ulikuwa wa duara. Macho yake yalikuwa kama yaliyotiwa wanja. Pua ndefu, midomo mizuri, mwenye ndevu nyingi. Alikuwa akinukia harufu nzuri. Ukimshika mikono yake ni laini.

Anas bin Malik anasema: “Sijawai kunusa ambari, wala kunusa miski, wala kitu chochote chenye harufu nzuri kushinda harufu ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Wala sijawahi kushika kabisa mkono wowote ulivyokuwa laini kuliko mkono wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie.”

Alikuwa Mtume mwenye uso wa bashasha, mara nyingi akitabasamu. Alikuwa ana sauti nzuri na alikuwa ana maneno machache.

## Tabia za Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa shujaa zaidi katika watu, amesema Ally bin Twalib Allah Amuie Radhi: “Tulikuwa tukipatwa na shida, na wakakutana watu kukutana na wengine basi tunajikinga kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie”.

Mtume alikuwa ni mwenye kutoa sana, hajaombwa kitu na mtu kisha akasema sina. Alikuwa mpole sana, alikuwa halipizi kisasi na wala hakasiriki, isipokuwa yakifanywa mambo ambayo yanavuka mipaka ya Allah basi anakuwa ni mwenye kulipiza kisasi kwa ajili ya Allah. Mtu wa mbali na wa karibu mwenye nguvu na dhaifu wote katika haki ya Allah kwake ni sawa

sawa. Kwa sababu hakuna mbora mbele ya Allah isipokuwa Mchamungu, kwani watu wote wako sawa. Na kwamba sababu ya kuangamia nyumati zilizotangulia ni kuwa akiiba mnyonge anasimamishiwa adhabu lakini akiiba mtukufu anaachwa. Mtume Rehema na Amani Zimfikie akasema: *"Wallahi hakika Fatuma bint Muhammad angeiba ningemkata mkono wake."*

Hakuwa Mtume ni mwenye kukitia dosari chakula, akikipenda atakula na akiwa hakitaki atakiacha. Familia yake ilikuwa ikipita mwezi au miezi miwili hakuwaki majumbani mwao moto, hakika chakula chao kikuu kilikuwa ni tende na maji. Alikuwa akifunga tumboni mwake jiwe au mawe mawili kutokana na njaa. Alikuwa akivisafisha viatu vyake na alikuwa akizishona nguo zake zilizochanika. Na alikuwa akiwasaidia wakeze kazi za nyumbani. Na alikuwa akiwazuru wagonjwa. Alikuwa Mtume ni mnyenyekevu zaidi kuliko mtu yeyote. Alikuwa akiitikia wito wa mtu yeyote awe tajiri au masikini. Alikuwa akiwapenda masikini na akihudhuria kwenye majenenza yao. Na akiwazuru wagonjwa bila ya kubagua. Alikuwa hamdharau fakiri kwa ufakiri wake, wala alikuwa hamuogopi Mfalme kwa ufalme wake.

Mtume alikuwa akipanda farasi, ngamia, punda na nyumbu.

Mtume alikuwa ni mwingi wa kutabasamu, alikuwa ni mzuri sana mwenye bashasha, pamoja na yale mengi yanayompata yenye kuhuzunisha. Alikuwa Mtume ni mwenye kupenda manukato, alikuwa akichukia harufu mbaya. Allah Amemkusanyia tabia njema zote na vitendo vizuri. Allah Amempa Mtume Wake Elimu ambayo Hakumpatia yeyote katika viumbe Wake wa mwanzo na hata wa mwisho. Alikuwa Mtume hajui kusoma wala kuandika. Alikuja na hii Qur'an itokayo kwa Allah Ambaye Amesema ndani yake;

*"Sema Ewe Muhammad kuwaambia hao, lau wataafikiana majini na binaadamu kujaribu kuleta mfano wah ii Qur'ani hawataweza kuileta, hata kama watashirikiana na kusaidiana kufanya hivyo."* (Al-Isra: 88)

Na Mtume alikulia hali ya kuwa hajui kusoma wala kuandika, alikata mzizi wa wale waliosema kuwa Muhammad ameiandika mwenyewe Qur'an au amejifunza au amesomeshwa kutoka katika vitabu vya kale.

## Miongoni mwa Miujiza ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Hakika miongoni mwa miujiza ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie ni Qur'an. Muujiza ambao utabakia mpaka siku ya kiyama. Muujiza ambao wameshindwa wenye fasaha ya maneno kuuelewa, wakashindwa watu wa balagha. Allah Akawapa changamoto wale wote ambao waliipinga Qur'an kuwa walete sura kumi zinazofanana na Qur'an au walete sura moja tu au walete aya moja tu mfano wa Qur'an. Washirikina wakashindwa kufanya hivyo.

Miongoni mwa muujiza wa Mtume siku moja waltaka washirikina kuwa awaletee alama moja tu ya kuthibitisha utume wake. Mtume akawaonyesha kupasuka kwa mwezi vipande viwili. Na kutoka maji kwenye vidole vyake mara nyingi sana. Na kutoa tasbihi kijiwe kwenye mkono wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie, kisha akakiweka kwenye kiganja cha Abubakar, kisha kwenye kiganja cha U'mar, kisha kwenye kiganja cha Uthman kisha kikasabihi.

Walikuwa wakisikia tasbihi ya chakula kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie hali ya kuwa anakula chakula. Na kusalimiwa na jiwe na miti na kuzungumzishwa na mfupa wa nyama ya mbuzi

iliyotiwa sumu na mama wa kiyahudi aliyetaka kumuua Mtume Rehema na Amani Zimfikie kwa sumu.

Mtume aliulizwa na Mbedui mmoja kuwa amuonyeshe alama ya kuthibitisha juu ya utume wake. Mtume akayapangusa matiti ya mbuzi ambayo hayakuwa na maziwa. Punde tu baada ya kushikwa, maziwa yakakusanyika, wakakamua maziwa wakanywa na akanywa maziwa hayo pia

Abubakar.

Alipatwa na ugonjwa wa macho Ally bin Abi Twalib, Mtume Rehema na Amani Zimfikie akayatabania macho yake na akapona kabisa. Alipatwa na tatizo mmoja wa Maswahaba zake Mtume, akawa hawezi kutembea, Mtume akampangusa akapona muda huo huo. Na akamuombea dua Anas bin Malik kuwa Mungu ampatie umri mrefu na awe na mali nyingi na watoto wengi na Allah Akambariki katika hali yake hiyo. Alizaa watoto mia moja na ishirini na ilikuwa mitende yake ikizaa kwa mwaka mara mbili, kwa kawaida mitende inazaa kwa mwaka mara moja. Na aliishi Anas miaka mia moja na Ishirini. Na siku moja, mmoja wa Maswahaba alimshitakia Mtume kuhusu ukame, hali yakuwa Mtume akiwa juu ya mimbari

yake. Akanyanyua mikono akamuomba Allah, muda mfupi mawingu yakakusa-nyika mfano wa Jabali, ikanyesha mvua nyingi sana. Wiki nzima kuanzia siku ya Ijumaa mpaka Ijumaa nyingine mpaka watu wakashitakia kuwa mvua imezidi sana. Mtume akamuomba Mola wake mvua ikakatika wakatoka watu kwenda kuota jua.

Walikula watu waliochimba handaki pishi moja na mbuzi mmoja ikawatosha watu wote wakashiba wakaondoka na wala chakula hakikupungua kitu. Na pia watu wa handaki walikula tende kidogo sana alizozileta bint yake Bashir bin Sa'ad kumletea baba yake na mjomba wake. Aliwalisha jeshi lilolikuwa na zawadi kutoka kwa Abu Huraira mpaka wakashiba. Wakatoka watu kumi na mbili kutoka kwa Maquraishi na hali ya kuwa wakiwaangalia ili wamuue akawa-mwagia mchanga kwenye nyuso zao akaondoka wala hawakumuona.

Mtume alifuatiliwa na Suraqa bin Malik kutaka kumuua. Wakati anamkaribia Mtume, akamuombea dua mbaya farasi wake, *Suraqa* akadidimia ardhini akashindwa kumfikia Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

## Maukifu ya Mtume na Mazingatio Katika Mwenendo Wake.

### Mizaha Yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Alikuwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie akiwafanyia mswahaba wake mizaha mbali mbali lakini alikuwa hasemi nao isipokuwa maneno ya haki. Mtume alikuwa akicheza na wakeze, akijiusisha zaidi na wale wenye umri mdogo, na alikuwa akifanya kama sehemu ya maisha yake, akiamiliana nao kwa yale yenye uwezo nayo na wanayoyafahamu.

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa akimfanyia mzaha mtumishi wake Anas bin Malik, wakati mwingine alikuwa akimwambia kwa mzaha: *"Ewe mwenye masikio mawili."* Alikuja bwana mmoja kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie akamwambia; "Ewe Mtume wa Allah nibebe." Mtume akamjibu kwa kumfanyia mzaha: *"Hakika yetu tutakubeba juu ya mtoto wa ngamia."* Yule bwana akasema: "Nitafanya nini juu ya mtoto wa ngamia?" Mtume akamjibu: *"Ngamia hazai isipokuwa anazaa mtoto wa ngamia."*

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa ni mwenye kutabasamu mara nyingi, na alikuwa ni

mwenye uso wa bashasha kwa maswahaba zake, hawamsikii kutoka katika kinywa chake isipokuwa maneno mazuri tu.

Jarir Allah Amuie Radhi amepokea: "Hakunizuia Mtume Rehema na Amani Zimfikie tokea niliposilimu na wala hajawai kuniona isipokuwa anaona tabasamu kwenye uso wangu. Kuna siku nikamshitakia Mtume Rehema na Amani Zimfikie ya kuwa mimi sikai vizuri kwenye farasi wangu (nadondoka) Mtume Rehema na Amani Zimfikie akanipiga piga kifuani kwangu akaniombea akasema; *"Ewe Allah mfanye huyu akae vizuri kwenye farasi wake (athibiti asidondoke) na mjaalie awe kiongozi mwenye kuongoza"*, sijawahi kudondoka baada ya dua ya Mtume."

Kama vile alivyokuwa Mtume akiwafanyia mzaha watu wake wa karibu, siku moja alikwenda nyumbani kwa bint yake Fatuma alipofika hakumkuta mumewe Ally bin Abi Twalib nyumbani, akamuuliza binti yake yuko wapi, akamjibu: "Kulikuwa kati yangu na yeye kuna kitu akanikasirisha basi akatoka." Akamjia Mtume akamkuta amejilaza msikitini, akawa amevua kilemba chake kiliingiwa na mchanga akawa anakifuta ule mchanga

huku akisema haya maneno; *"Simama baba wa Mchanga simama baba wa mchanga."*

## Kuamiliana Mtume Rehema na Amani Zimfikie na Watoto.

Kwa hakika watoto wamekuwa na nafasi kubwa katika tabia njema, alikuwa Mtume akishindana na mkewe Aisha Allah Amuie Radhi alikuwa Mtume akimruhusu kucheza na marafiki zake katika utotoni.

Mama Aisha anasema: "Nilikuwa nikicheza na mabinti kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie, na nilikuwa na marafiki zangu niliokuwa nikicheza nao, alikuwa Mtume akija wanajificha asiwaone, basi alikuwa akiwatuma kuja kucheza na mimi."

Kama ambavyo Mtume alikuwa akijihusisha sana na watoto na akicheza nao na akiwafanyia mema. "Alitutokea siku moja Mtume Rehema na Amani Zimfikie katika moja ya Swala yangu ya Ishaa, na akiwa amembeba Hassan au Hussein (moja ya wajukuu zake) akapita mbele kuswalisha akamuweka chini kisha akapiga takbira ya kuhirimia Swala akaswali, akasujudu sijida ndefu sana. Baba yangu akasema: "Nikanyanyua kichwa kuangalia, nikamuona mtoto yupo juu ya mgongo wa Mtume

amepanda hali ya kuwa Mtume amesujudu. Anasema; "Nikarudi kwenye sijida yangu, alipomaliza Mtume Swala watu wakamuuliza: "Ewe Mtume wa Allah, hakika umesujudu sijda ndefu sana mpaka tukadhani kuwa kuna jambo limetokea au unateremshiwa wahyi." Mtume akasema: *"Hayo yote siyo, mtoto wangu alinipanda mgongoni nikaona sio vema kumuwahisha kumshusha mpaka amalize mambo yake ndipo ashuke."*

Anas bin Malik anasimulia kuwa: "Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa ni mwenye tabia nzuri kushinda mtu yeyote, alikuwa akimuita mdogo wangu: *"Ewe Abu Umeir, amefanya nini ndege mdogo?"* Alikuwa ana ndege wake mdogo akimchezea chezea huyu mtoto. Mtume alikuwa akimliwaza huyu mtoto."

## Muamala Wake Mtume kwa Wakeze.

Muamala wake Mtume Rehema na Amani Zimfikie na wake zake ulikuwa umekusanya tabia njema na mafundisho mbali mbali. Alikuwa Mtume ni mwenye unyenyekevu na alikuwa siku zote akiwahitajia wake zake. Mwanamke alikuwa ana nafasi kubwa kwake kama mwanadamu, mama na mke na binti. Siku moja bwana mmoja alimuuliza Mtume Rehema na Amani

Zimfikie: "Ni nani mwenye haki zaidi kumfanya kuwa rafiki yangu wa karibu?" Mtume akamjibu: "*Mama yako.*" Akauliza: "Kisha nani?" Mtume akamwambia mara ya pili: "*Mama yako*." Akauliza tena mara ya tatu: Mtume akamwambia "*Mama yako. Kisha baba yako.*"

Mtume pia amesema, "*Yeyote ambaye atawakuta wazazi wake wawili bado wako hai au mmoja wao yuko hai, akaacha kuwafanyia wema na akafa ataingia motoni na Allah Atamuweka mbali naye".*

Na alikuwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie akinywa na mke wake kwenye chombo alichonywea mkewe na yeye anakunywa pale pale uliponywea mdomo mkewe na alikuwa akisema: "*Mbora wenu ni yule mbora kwa wakeze na mimi ni mbora wenu kwa wake zangu.*"

## Huruma Yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Kuhusu huruma ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie kwa hakika anasema: "*Wenye kuwa na huruma Anawahurumia Allah, wafanyieni huruma waliopo ardhini Atawafanyia huruma waliopo mbinguni."*

Mtume wetu mtukufu mkarimu ana nafasi kubwa katika hii tabia tukufu, tabia zake tukufu zinadhihirika wazi wazi katika jamii kuanzia kwa watoto mpaka kwa wakubwa kwa wa karibu mpaka kwa wa mbali.

Miongoni mwa huruma zake mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa akihafifisha Swala yake haifanyi kuwa ndefu wakati akisikia mtoto analia.

Hadithi ya Abi Qatadah Allah Amuie Radhi, Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Hakika yangu ninasimama kwenye Swala kwa lengo la kutaka kuirefusha, nikisikia mtoto analia, naibadilisha Swala yangu kwa kuchukia kumpa tabu mama yake".*

Na kwa kuhurumia umma wake, na kuwa na pupa juu yao ili waingie katika Dini ya Allah, siku moja aliumwa kijana mmoja wa kiyahudi aliyekuwa akimuhudumia. Mtume Rehema na Amani Zimfikie akaenda kumtembelea na kumsalimia. Mtume akakaa kichwani kwake, akamwambia: "*Silimu*." Yule kijana akamuangalia baba yake aliyekuwa amesimama kichwani kwake. Baba yake akamwambia mwanaye: "Mkubalie Abal Qassim." Yule kijana akasilimu, kisha hakukaa muda mrefu yule kijana akafariki, akatoka Mtume kwa yule kijana huku akisema: *"Namshukuru Allah ambae amemuokoa kijana huyu na moto."*

## Kusubiri Kwake Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Kuhusu maelezo ya subira yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie ni mengi. Kwani maisha yake yote Mtume Rehema na Amani Zimfikie ni subira na kuhusiana kusubiri, na kupigana jihadi na kuhimiza jihadi. Na Mtume akawa anaendelea kusubiri na kuhimiza kusubiri, na kufanyia kazi ya kuunganisha watu tokea iliposhuka aya ya mwanzo, mpaka dakika ya mwisho ya maisha yake.

Kwa hakika Mtume Rehema na Amani Zimfikie alifahamu tabia ambazo atakutana nazo katika njia ya da'awa. Kutokea mwanzo wa kutumilizwa na baada ya kukutana na Malaika Jibrili *Alayhi ssalam* wakati alipokwenda kwa mama Khadija Allah Amuie Radhi. Bi Khadija alimpeleka kwa Waraqat bin Naufal, na Waraqa alisema: "Natamani ningelikuwa hai wakati wakikufukuza na kukutoa ndugu zako kutoka mjini kwako." Mtume Rehema na Amani Zimfikie akamuuliza: *"Wao watanitoa mjini kwangu?"* Waraqa akamjibu: "Ndio, kwani haji mtu yeyote mfano wako na mambo kama uliyokuja nayo wewe isipokuwa atafanyiwa uadui."

Akajituliza Mtume Rehema na Amani Zimfikie tokea mwanzo alipoanza kubeba matatizo, maudhi, vituko na uadui kutoka kwa watu wake.

Miongoni mwa misimamo ambayo inaonyesha uzuri wa subira zake Mtume Rehema na Amani Zimfikie ni yale yaliyomdhihirikia kutokana na maudhi ya kimwili kutoka kwa watu wake na jamaa zake. Naye akiwa katika mji wa Makkah akifikisha ujumbe wa Allah. Katika hayo ni yale ambayo ameyaeleza Imamu Bukhari katika Hadithi aliyoipokea A'rwah bin Zubeir Allah Amuie Radhi:

"Hakika A'rwah bin Zubeir alimuuliza Abdullah bin A'mri bin A'aswi kuwa ni kitu gani kibaya kikubwa walicho kifanya washirikina kumfanyia Mtume Rehema na Amani Zimfikie, akamjibu: "Wakati akiwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie akiswali Al-Ka'aba, muda mfupi akajiwa na U'qbah bin Abi Mui'twi akaiweka nguo yake kwenye shingo ya Mtume, akamnyonga kwa nguvu sana, akatoka Abubakar akamshika kwenye mabega yake na akamuokoa Mtume na kumwambia U'qubah: "Mnamuua mtu ambaye anasema Mola wangu ni Allah?"

Siku miongoni mwa masiku alikuwa Mtume akiswali kwenye Ka'aba. Abu Jahal na wenzie wakiwa wamekaa, wakaambiana ni nani atakayeleta uchafu wa matumbo ya ngamia na kumwagia mgongoni mwake Muhammad wakati akiwa anasujudu. Wakamtuma kijana mmoja muovu wao akaja nayo, wakamsubiri mpaka aliposujudu Mtume Rehema na Amani Zimfikie wakamuwekea juu ya mgongo wake, kati ya mabega yake. Wakawa wanacheka kwa furaha huku wakiangukiana huku na huku. Na Mtume Rehema na Amani Zimfikie ni mwenye kusujudu. Hajanyanyua kichwa chake mpaka akajiwa na bint yake Fatima akauondoa ule uchafu kutoka kwenye mgongo wake.

Na katika mambo mabaya zaidi ni kumtuhumu Mtume na sifa mbaya ambazo zinaudhi nafsi katika kuipinga da'awa yake na kumkadhibisha kuwa sio kweli. Ni kumtuhumu kuwa Kuhani, ni Mshairi, ni Mwenda wazimu na ni Mchawi, na kudai kuwa hayo yote aliyoletewa katika alama na Aya ni ngano za watu wa kale na sio kweli. Na miongoni mwa hayo mambo ni yale aliyoyasema Abu Jahali hali ya kumfanyia Mtume istihizai na dharau ni haya; "Ewe Allah ikiwa haya ni ya kweli kutoka Kwako basi

tunakuomba Ututeremshie jiwe kutoka mbinguni au Utuletee adhabu kali yenye kuumiza."

Na alikuwa A'mi yake Abu Lahab akimfuatilia kila anapokwenda kwenye mikusanyiko ya watu na kwenye masoko yao kwa lengo la kuwalingania kuingia kwenye Uislamu, anampinga na kumkanusha na kuwakataza watu wasimsadikishe na kumkubali Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Na alikuwa mke wake Ummu Jamil akikusanya kuni na miba akiitupa na kuiweka katika njia anayopita Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Maudhi yalifikia hali ya juu pale alipozingirwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie na Maswahaba zake kiasi cha miaka mitatu katika sehemu ya bonde la Abu Twalib, mpaka ikafikia wanakula majani ya miti kutokana na njaa kali. Na ikawa huzuni imezidi pale alipompoteza A'mi yake ambaye alikuwa akimkinga na maudhi ya Maquraishi. Na huzuni ikamzidi kwa kuwa A'mi yake alikufa katika hali ya ukafiri. Na ghafla akafiwa na mke wake, mama Khadija Allah Amuie Radhi, ambaye alikuwa akimliwaza mara nyingi kutokana na maudhi ya Maquraishi.

Kutoka kwa Anas amesema: Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: "*Kwa hakika*

*nimetishwa kwa ajili ya Allah hakuna yeyote aliyetishwa zaidi yangu, hakika niliudhiwa kwa ajili ya Allah hakuna yeyote aliyeudhiwa zaidi yangu. Ilinichukua siku thelathini mchana na usiku, na mimi na Bilal hatuna chakula ambacho mtu mwenye ini anaweza kula, isipokuwa kitu ambacho Bilal alichokificha chini ya kwapa lake."* Maana ya Hadithi hii ni pale Mtume alipokimbia kutoka Makka pamoja na Bilal. Bilal hakuwa na chakula chochote alichokuwa amekibeba ili kilichopo chini ya mkono wake.

Kwa hakika Mtume Rehema na Amani Zimfikie alituhumiwa katika heshima yake, yalimkuta maudhi mengi kutoka kwa wanafiki na mabedui wajinga;

Hadithi aliyoipokea Imamu Bukhari kutoka Abudullah bin Mas'udi Allah Amuie Radhi anasema: "Mtume Rehema na Amani Zimfikie, aligawa ngawira. Bwana mmoja katika Answar akasema: "Wallah Muhammad kwenye mgawanyo huu hakufanya kwa ajili ya Allah." Akasema Ibn Mas'udi: "Nikamuendea Mtume Rehema na Amani Zimfikie nikamsimulia, ukabadilika uso wake na akasema Mtume: *"Allah Amrehemu Mussa, kwa hakika aliudhiwa zaidi ya haya na akasubiri."*

Katika sehemu ambazo Mtume Rehema na Amani Zimfikie alipata huzuni kubwa ni siku ambazo walikufa watoto wake wa kiume na kike, kwani alikuwa ana watoto saba, walikufa mmoja baada ya mmoja, ikafikia hakubakia katika watoto wake isipokuwa Fatima Allah Amuie Radhi. Lakini Mtume Rehema na Amani Zimfikie alisubiri subira nzuri. Mpaka ikapokewa kutoka kwake siku aliyokufa mtoto wake Ibrahim alisema: *"Hakika jicho linatoka machozi na moyo una huzunika, na wala hatusemi isipokuwa yale yanayomridhisha mola wetu, na hakika yetu kwa kuondoka ewe Ibrahim ni wenye kuhuzunika."*

Haikuwa subira ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie imejifupisha kwenye maudhi na mitihani pekee, bali subira yake ilikusanya pia kumtii Allah katika Amri Zake. Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikuwa akijitahidi katika Ibada na kumtii Allah mpaka miguu yake inavimba kutokana na kisimamo kirefu. Na alikuwa akifunga sana na kumtaja sana Allah na Ibada nyinginezo, alipoulizwa kuhusu hilo Mtume Rehema na Amani Zimfikie akasema: *"Hivi nisiwe mja mwenye kushukuru?"*

## Zuhudi Yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Hauwezi kusadikisha kuhusu kusifu zuhudu (kuipa nyongo dunia) kivitendo isipokuwa juu ya yule ambayo imekuwa kwake ni wepesi katika jambo miongoni mwa mambo, akapa nyongo dunia na kuiacha kabisa. Mtume wetu alikuwa ni mwenye kuipa nyongo dunia zaidi kuliko mtu yeyote katika hii dunia. Na alikuwa ni mchache katika kuipenda dunia. Alitosheka katika kuyafikisha yale ambayo Allah Alimtaka ayafikishe. Aliridhia katika maisha anayoishi, pamoja na kuwa dunia ilikuwa kwenye mikono yake. Na pamoja ya kuwa Mtume alikuwa kiumbe bora katika viumbe vya Allah. Na laiti Allah Angetaka kumpa Mtume Wake Angempa atakacho katika mali na neema mbali mbali.

Imamu Ibn Kathir katika tafsiri yake amesema; Hadithi ilipokelewa na Khaithama ya kwamba aliambiwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie: "Ukitaka Tutakupa katika hazina zote za Ardhi na funguo zake kiasi ambacho Hatujampatia Nabii yeyote kabla yako, wala Hatujampatia yeyote baada yako, wala hakutapungua chochote katika yale yaliyopo kwa Allah." Mtume akasema: *"Nikusanyieni* hiyo dunia kesho Akhera."

Kuhusu maisha ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie ni maisha ya ajabu sana, Abu Dharri Allah Amuie Radhi anasema: Nilikuwa nikitembea na Mtume kwenye ardhi yenye mawe huko Al-Madinah wakati wa mchana, alipouona Mlima wa Uhud. Mtume ﷺ akasema: 'Ewe Abu Dharr!' Nikasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hapa nakuitikia". Akasema: "Lau ningekuwa na dhahabu nyingi kama uzito wa Uhud, isingependeza kwangu kuwa na dinari moja ndani yake baada ya kupita siku tatu, sana sana ningezuia kitu kwa ajili ya kulipa deni. Ningeisambaza mali hiyo kwa waja wa Allah hivi na hivi na hivi. Na Mtume akawa anaashiria mbele yake, na upande wake wa kulia na wa kushoto."

Mtume ﷺ alikuwa akisema: *"Wapi na wapi mimi na dunia, haikuwa mimi na dunia isipokuwa kama mwenye kupanda juu ya kipando kisha akajipumzisha kwenye kivuli cha mti, kisha akaondoka akakiacha kivuli hapo hapo."*

## Chakula Chake Mtume na Mavazi Yake.

Kuhusu chakula chake Mtume ﷺ ilikuwa inaweza kupita mwezi mmoja au miezi miwili mpaka mitatu nyumbani kwake hakuwaki moto. Isipokuwa alikuwa akila vyeusi viwili yaani tende na maji. Kwani wakati mwingine anaendelea siku nzima amechoka

kutokana na njaa kali na anakosa cha kujaza tumbo lake. Ulikuwa mkate wake ni kutokana shayiri na vile vilivyopkelewa kuhusu Mtume Rehema na Amani Zimfikie kwamba alikula mkate mwembamba mara zote. Kwani mtumishi wake Anas Allah Amuie Radhi anaeleza kuwa haikuwahi kukusanyika kwa Mtume chakula cha milo miwili, mlo wa mchana na mlo wa usiku kutokana na mkate na nyama isipokuwa siku hiyo ametembelewa na wageni.

Haikuwa hali yake katika mavazi isipokuwa ni kidogo sana kama ilivyo tangulia. Kwa hakika wanashuhudia maswahaba wake Mtume kutokana na kuipa nyongo kwake dunia na kutojikalifisha katika mavazi ya kifahari hali yakuwa alikuwa anao uwezo wa kuvaa nguo za ghali sana. Mmoja wa maswahaba wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema akiwa ni mwenye kusifu nguo ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie:

"Nilikwenda kwa Mtume ﷺ kuongea naye kuhusu kitu fulani muda huo akiwa amekaa na amevaa nguo ya pamba iliyo nzito."

Aliingia siku moja swahaba wa Mtume aitwae Buraidah Allah Amuie Radhi kwa mama Aisha-Ummul Muuminiina, anasema: "Nikatoa nguo iliyochanganyi-

ka weupe na weusi na kikoi cha pamba nzito, kisha akasema mama A'isha: "Alipokufa Mtume alifunikwa na nguo hizi mbili."

Anas bin Malik Allah Amuie Radhi anasema: "Nilikuwa nikitembea pamoja na Mtume Rehema na Amani Zimfikie naye akiwa amejitanda kishali cha kutoka mji wa Najran chenye ncha nzito."

Na Mtume Rehema na Amani Zimfikie hakuacha wakati anakufa hata dirham moja wala dinari moja, wala hakuacha mtumwa wa kiume wala mtumwa wa kike wala chochote, isipokuwa alimuacha nyumbu wake mweupe na silaha yake, na ardhi aliitoa sadaka. Mama A'isha Allah Amuie Radhi akasema: "Alikufa Mtume Rehema na Amani Zimfikie hakuacha kwangu chochote anachoweza mtu kula mwenye njaa isipokuwa aliacha nusu ya shairi (ngano)."

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alikufa na *Dir'hi* yake (kofia ya kivita inayotengenezwa kwa chuma), aliiweka rehani kwa Yahudi ili ampatie chochote katika ngano (*shayiri*).

## Uadilifu Wake Mtume Rehema na Amani Zimfikie.

Kuhusu uadilifu wake Mtume Rehema na Amani Zimfikie ni katika kufanya muamala wake na Allah-Mola Mtukufu, kujifanyia uadilifu yeye mwenyewe, kafanya uadilifu kwa wakeze na kufanya uadilifu katika kuamiliana na watu wengine. Watu wa karibu au watu wa mbali. Awe ni rafiki au jamaa tu. Kufanya uadilifu kwa yule anayemkubali au asiyemkubali hata kwa adui mkubwa kwake, huyo ana nafasi ya kufanyiwa uadilifu kwake. Watu wanampinga, watu wanakosea katika haki yake, lakini Mtume hajitengi katika kuwafanyia uadilifu. Kwani uadilifu ni kitu cha lazima kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie kukifanya akiwepo au akiwa safari. Alikuwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie anachukia kuwabagua maswahaba zake, alikuwa akipenda uadilifu na usawa na alikuwa akibeba matatizo kama wao.

Hadithi ya Abdullah bin Masu'ud Allah Amuie Radhi anasema: "Tulikuwa siku za Badri tunapanda kila watu watatu ngamia mmoja na alikuwa Abu Lababah na Ally bin Abi Twalib wao wamekuwa pamoja na Mtume Rehema na Amani Zimfikie, ilipofika zamu ya Mtume kupanda kwenye ngamia wao wakamwambia

Mtume sisi tunatembea na miguu wewe panda kwenye huyu ngamia, Mtume akawaambia: *"Nyinyi hamkuwa ni wenye nguvu kunishinda mimi, wala mimi sikuwa ni mwenye kutosheka na malipo kulikoni nyinyi."*

Wakati Usaid bin Hudhair akiwafanyia mzaha watu na kuwachekesha, akasema kuwa Mtume amemuumiza sehemu za chini na fimbo yake, akasema Usaid: "Ulinitia maumivu na fimbo yako, nataka kulipiza kisasi kwako." Mtume akamwambia: *"Lipiza kisasi."* Usaid akamwambia Mtume: "Wewe umevaa kanzu na mimi sikuwa na kanzu." Mtume akainyanyua juu kanzu yake, Usaid akamkumbatia Mtume Rehema na Amani Zimfikie huku akimbusu tumboni mwake na sehemu za mbavu zake. Usaid akasema: "Hakika nilikuwa nataka hili ewe Mtume wa Allah (kukubusu tu)."

Na alikuwa Mtume ﷺ hapendi kuziacha kuzifanyia kazi hukumu za Allah ambazo Ameziweka ili kusimamisha uadilifu katika watu, na hata kama aliyefanya kosa ni katika jamaa wake wa karibu na vipenzi vyake.

Katika tukio la mwanamke mmoja wa kabila la Makhuzumiyya ambaye aliiba akaja kuombewa

msamaha na Usama, Mtume hakukubali alisema hukumu yake inafahamika, akasema: *"Enyi watu! Kwa hakika waliangamia waliokuwa kabla yenu, kwani walikuwa akiiba kwao mtu mwenye heshima kwao wanamuacha na akiiba mtu mnyonge kwao wanamsimamishia adhabu, naapa kwa Allah, laiti Fatima bint Muhammad angeiba basi ningemkata mkono wake."*

## Waliyoyasema Kuhusu Muhammad Rehema na Amani Zimfikie.

Yafuatayo ni miongoni mwa yaliyo okotwa okotwa kwenye maneno ya baadhi ya wanafalsafa na *Mustashirikuna* wa Kimagharibi katika kumzungumzia Mtume Muhammad Rehema na Amani Zimfikie. Wakibainisha kutambua kwao utukufu wa Mtume na utume wake aliopewa na Allah pamoja na sifa nzuri alizokuwa nazo na ukweli kwa yale aliyokuja nayo. Akiwa mbali na ubinafsi, na kuenezwa kwa maneno ya batwili yasiyokuwa ya kweli kwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie kutoka maadui wa Uislamu.

Muingereza **Bernad Show** anasema katika kitabu chake kuhusu Mtume Muhammad, kitabu ambacho kilichomwa na utawala wa Uingereza:
"Hakika Dunia inahitajia mambo ambayo kama aliyoyafanya Muhammad katika kufikiria. Huyu ni Mtume ambaye aliiweka Dini yake katika heshima na utukufu. Kwani ndio Dini yenye uwezo katika dini zote katika miji. Itabakia Dini hii milele. Na hakika mimi ninawaona watu wengi wakiingia kwenye hii dini kwa uwazi na dalili. Na dini hii itapata nafasi pana katika bara la Ulaya."

Na anasema kuwa: "Hakika viongozi wa dini katika karne za kati kati, kwa sababu ya ujinga na ubinafsi, waliandika kuhusu Dini ya Muhammad,

wakazidisha mambo mengi, wakawa wanamuhesabu kuwa ni mtu aliyekuja kupiga vita Ukiristo, lakini mimi nimemsoma huyu mtu kuwa ni mwenye maajabu makubwa. Nikapambaukiwa kuwa hakuja kuupiga vita Ukiristo, bali inafaa kuitwa kuwa ni Mkombozi wa wanadamu wote. Kwa rai yangu ninaona kuwa kama angepewa dunia hii ya sasa hivi, angeweza kutatua matatizo yetu tuliyokuwa nayo kwa kuleta Amani, salama na mafanikio ambako kila mwanadamu anakutegemea."

Mwanafalsafa wa Kiingereza **Thomas Korlyl** aliyepata tuzo ya Nobel, anasema katika kitabu chake kuhusu Mashujaa: "Kwa hakika imekuwa ni aibu kubwa kwa kila mtu katika zama hizi kusikiliza yasemwayo kwamba Dini ya Uislamu ni uongo na kuwa Muhammad ni mwenye kufanya hadaa na hila. Kwa hali hii ni wajibu kupiga vita kila linalotangazwa, mfano wa haya maneno mabaya tena maovu. Hakika ujumbe ambao alioutekeleza Mtume bado unaendelea kuwa ni taa yenye kuangaza kiasi cha karne kumi na mbili, mfano wa watu Milioni mia mbili. Hivi mmoja wenu anaweza kudhania kuwa ujumbe ambao aliishi nao na akafa juu yake na Mamilioni wakaufuata kwa kushikamana nao ni uongo na hila?" Mwanafalsafa **Raamah Krishna Row** anasema: "Wakati alipokuja Muhammad katika kisiwa cha Waarabu hapakuwa ni kitu chenye kutajwa, kutokana

na jangwa ambalo hakuna kitu. Aliweza Muhammad kwa bidii yake na roho yake kubwa kuanzisha Dunia mpya na maisha mapya na utamaduni mpya na ustaarabu mpya. Akaanzisha mamlaka mpya iliyopanuka kuanzia Moracus mpaka bara Hindi, na akaweza kuathiri fikra na maisha ya mabara matatu ambayo ni Bara la Asia, Bara la Afika na Bara la Ulaya.

Mustashriki **Kenedy Zuweymir** anasema, "Hakika ya Muhammad kweli alikuwa mtu mzuri hakuna shaka, ni katika viongozi wakubwa wa dini, akisadikisha maneno yake aliposema: 'Hakika ya Muhammad alikuwa ni mwenye kutengeneza mambo na anao uwezo, mfikishaji mwenye fasaha, mwenye ushujaa wa kupigana vita vingi, mwenye fikra nyingi, haifai kumnasibisha na sifa ambazo zinazopingana na sifa hizi. Na Qur'an yake ambayo amekuja nayo na mwenendo wake vinashuhudia kukubalika madai haya."

Muingereza **Sir William Muir** anasema, "Hakika ya Muhammad ambaye ni Nabii wa Waislamu alipachikwa jina la Muaminifu tokea udogoni mwake kwa makubaliano ya watu wote wa mji wake. Kwa utukufu wa tabia zake, na mwenendo wake mzuri. Vyovyote vile hali ilivyo, kwa hakika Muhammad anayo sifa iliyotukuka ya hali ya juu, hakuna anayeweza kuielezea kwa utukufu wake. Na ni

mwenye ujuzi kutokana na maono katika Historia yake tukufu. Hiyo ni Historia ambayo imemuacha Muhammad kuwa ni mwanga wa Mitume na Mtafiti Mkuu wa Dunia."

Na anasema tena: "Hakika Muhammad alifaulu kwa uzuri wa maneno yake, na wepesi wa Dini yake, na hakika kazi zake zilitimia kwa yale yanayoishitua akili. Historia haikuweka mafungamano ya kuziamsha nyoyo na kuhuisha tabia na kunyanyua ubora katika muda mfupi kama alivyofanya Nabii wa Waislamu ambaye ni Muhammad."

Mwandishi mmoja wa vitabu na Mwanafalsafa wa Kirusi **Tolestoway** anasema, "Inatosha Muhammad kujifaghari ya kwamba alimaliza kwa Umma wake udhalilifu unaotokana na makucha ya shetani ya mazoea mabaya, na akafungua mbele yao njia ya maendeleo na kupiga hatua mbele. Hakika sharia ya Muhammad itauongoza Ulimwengu kwa kuukusanya kwa kutumia akili na hekima."

Muaustralia ***Shibrak***: anasema, "Hakika ubinadamu ni kule mtu kujifagharisha na kujinasibisha na mtu kama Muhammad, pamoja na kwamba hajui kusoma wala kuandika, lakini aliweza kabla ya karne ya kumi kuwaletea watu sharia. Tutakuwa sisi watu wa Ulaya watu bora zaidi kwa yale tutakayokuwa nayo, pindi tukifikia hali ya juu zaidi."

# Fihrisi ya Kitabu

Hali za Waarabu Kabla ya Mtume Kutumwa: .........3
Kisa cha Tembo. ..............................................6
Kunyonyeshwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie. 8
Tukio la Kupasuliwa Kifua. ................................11
Utume. ...........................................................15
Kulingania kwa Wazi. .......................................18
Kuhama Kwenda Habasha. ................................21
Mwaka wa Huzuni. ...........................................24
Mtume Yupo Twaif. ..........................................25
Kupasuka kwa Mwezi. ......................................27
Israa na Mi'iraji. ..............................................27
Kituo Kipya cha Da'awa. ...................................31
Mtume Rehema na Amani Zimfikie Yupo Mji wa Madina. ........................................................36
Vita Vya Badri. ................................................37
Vita vya Uhud. ................................................39
Vita vya Handaki. .............................................40
Kuukomboa Mji wa Makkah. .............................41
Makundi Kuja kwa Mtume na Kuwaandikia Barua Wafalme. .......................................................42
Kifo cha Mtume Rehema na Amani Zimfikie .........44
Sifa ya Mtume Kimaumbile. ...............................45
Tabia za Mtume Rehema na Amani Zimfikie. ........46
Miongoni mwa Miujiza ya Mtume Rehema na Amani Zimfikie. ....................................................49

Maukifu ya Mtume na Mazingatio Katika Mwenendo Wake. .......................................................... 52
Mizaha Yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie. .. 52
Kuamiliana Mtume Rehema na Amani Zimfikie na Watoto. ....................................................... 54
Muamala Wake Mtume kwa Wakeze. .................. 55
Huruma Yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie. 56
Kusubiri Kwake Mtume Rehema na Amani Zimfikie. ............................................................ 58
Zuhudi Yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie. .. 64
Chakula Chake Mtume na Mavazi Yake. ............... 65
Uadilifu Wake Mtume Rehema na Amani Zimfikie. 68
Waliyoyasema Kuhusu Muhammad Rehema na Amani Zimfikie. ............................................... 71